



## KILIMO CHA KARAFUU



### Utangulizi

Kuna ukuaji mkubwa wa mahitaji ya mazao ya viungo duniani ingawa uzalishaji na uuzaji wa viungo ni wa chini pamoja na kuwa na maeneo mazuri ya uzalishaji. Ikiwa uzalishaji utakuwa na ubora hasa matumizi ya mbegu bora na kilimo kisichotumia mbolea za viwandani soko lake ni ufumbuji kwa mkulima. Soko la nje ni kama Afrika ya kati, Asia, Ulaya, Afrika na Amerika. Soko la ndani linajumuisha Zanzibar na Tanzania Bara.

### Kilimo bora cha karafuu

- Karafuu ni zao linalotumika katika matumizi mbalimbali yakiwemo viungo vya vyakula na vinywaji na kujumuisha katika michanganyiko ya madawa ya aina mbalimbali.
- Zao hili pia hukamuliwa mafuta ambayo yanatumka kama dawa na kuongeza harufu mzuri katika manukato ya mapambo. karafuu ni moja ya mazao machache ambayo thamani

kubwa iko katika maua yake, zao lingine ni pareto.

### **Vitalu vya karafuu**

Viko vitalu vya aina mbili:-

#### **1. Kutumia matuta ya kawaida**

matuta ya **sentimita (sm) .120** hutengenezwa na kuyaweka mbolea ya samadi na kisha mbegu hupandwa katika sehemu mbili za tuta kwa nafasi ya cm. 15 – 20 kati ya mimea. Hadi ifikie umri wa miezi 4-6 ndipo upandikize. Wakati wa kupandikiza hakikisha usiukate mzizi wa katikati vinginevyo miche mingi itakufa. Andaa kitalu ili wakati wa kupandikiza uwe mwanzo wa mvua nyingi.



*Kitalu kwa Kutumia matuta*

#### **2. Kutumia viriba**

- Njia hii ni nzuri zaidi kwani inalinda mzizi mkuu usiharibike wakati wa kupandikiza.
- Udongo wa msituni, samadi na mchanga kwa ujazwe kwenye kiriba kwa uwiano wa 3:2:1.
- Jengea kichanja na mwagilia maji hadi mbegu zoite
- Miche ipeleke shambani baada ya miezi 4-6.



*Kitalu kwa Kutumia viriba*

**Mazingira ambayo karafuu hustawi.**

**Hali ya joto**

- kiasi cha nyuzijoto 27 – 30
- lakini Tanzania bara hadikati ya nyuzijoto 24-30.

**Mwinuko kutoka usawa wabahari**

- Kuanzia mita 50 -1000
- ingawa kuanzia mita 700 – 800 maua yanajitokeza upesi.

**Mvua**

- Mvua kiasi milimita 1500-3000 kwa mwaka

**Udongo**

- udongo wenye rutuba na tifutifu ili mizizi ipenye kwa urahisi ardhini. Sehemu zenye mawe mawe au rutuba chache mikarafuu hufa ikiwa mikubwa.

**Uvumilivu wa ukame**

- Mikarafuu midogo haina uvumilivu na wakati wa ukame mara nyingi hukauka na kufa hivyo baadhi yamaeneo ya pwani ya bara ni vigumu kustawisha karafuu ikiinganisha na visiwani kwa sababu visiwani unyevu wa bahari huwa karibu zaidi

### **Utayarishaji wa shamba**

- Shamba liwe safi na ni wajibu kuchimbua visiki ili kuzuia maradhi yatokanayo na vimelea vya ukungu.

### **Mbeguza karafuu**

- Mbegu hutokana na matunda yaliyokomaa ambayo huitwa mabibo.
- Wakati wa kuchuma ni vizuri kubakiza tawi moja litakomaa hadi kutoa mabibo yawe kama mbegu.

### **Uchaguzi wa mbegu**

- Tumbukiza mabibo kwenye ndoo ya lita 10 za maji yaliochanganywa na sukari kiasi cha robo kilo. Mbegu zitakazozama ndizo za kuchukuliwa kuweka kitaluni.

### **Nafasi na upandaji**

- Umbali kati ya mti na mti ni mita kumi kwa kumi (10 X 10) hadi mita 12 X 12.
- Upandaji huu utatoa nafasi ya kupanda mazao mengine.



### **Mashimo**

- Yachimbwe kwa vipimo vya sm 60 kwa 60 na yaachwe wazi kwa miezi 2, ili kuuwa vimelea vya ukungu na minyoo inayoharibu mizizi.

- Kabla ya kupanda changanya udongo wa juu na mbolea yasamadi iliyooza debe moja kila shimo na panda mwanzoni mwa mvua za masika.

#### **Utunzaji**

- Palilia na wekea matandazo kwa miche michanga hadi itakapo kua.
- Kama eneo lina jua sana ni vizuri kupanda migomba iwe na kivuli cha wastani kuzuia joto kali katika mizizi.
- Endelea na palizi kwa muda wote wa karibia miaka 4-5 ambapo karafuu inanza kuzaa.

#### **Kuchanganya na Mazao Mengine**

- Mkulimaanashauriwa kupanda mazao ya muda mrefu na ya muda mfupi katika shamba lake la mikarafuu, kufanya hivyo kunasaidia kumpa hamu na muda Mkulima kulihudumia vyema shamba lake.

#### **Uvunaji**

- Kinachovuna ni maua na huvunwa pale yanapochanua kabla ya kuweka bibo, kwani huwa likiweka bibo basi mafuta yanayohitajika hutoweka na thamani yake hushuka.
- Huvunwa kwa kuupanda juu na kutoa vikonyo vya mauwa.
- Mti mkubwa kati ya 10-20kg na kwa Zanzibar hutoa hadi kilo 25 kwa mti.

**Imeandaliwa na**

**Kitengo cha Utafiti wa Viungo TARI-Mlingano,**

**S.L.P 5088, TANGA.**

**Simu: +255 688 150 745**

**Barua pepe: [cdmlingano@tari.go.tz](mailto:cdmlingano@tari.go.tz)**



*Karafuu iliyovunwa*

#### **Kuanika karafuu na kupanga madaraja:**

- Huanikwa juani hadi zinakauka. Madaraja yapo karibu ya matano ila Tanzania bara lipo daraja moja.



*Karafuu iliokaushwa*

#### **Soko la karafuu**

- Soko la karafuu lipo kwa kupitia mashirika binafsi.
- Kilo moja ya karafuu huuzwa kati ya Tzs 9000-16,000 kutegemeana na msimu

#### **Faida ya karafuu**

- Faida za kiafya, husaidia kwenye mmeng'enyo wa chakula.
- kuimarisha mfumo wa kinga mwilini, na kudhibiti ugonjwa wa kisukari.
- Karafuu Huzuia visababishi vya kansa (*anti-mutagenic properties*) sambamba na kupambana na magonjwa ya kinywa.